

*Shairi lifuatalo liliandikwa na Malenga Hamidu Tambwe miaka kadha iliyopita likizungumzia umuhimu wa utunzi mzuri wa mashairi na nasaha za kimaisha*

### UTENZI

1. Kwamba utenzi kutenda, mtu ukajitendea,  
Siyo kupiga kandanda, au nyundo kutumia,  
Japo iwe ni kuenda, mguu ukitumia,  
Huyo amepanda punda, utenzi kamalizia.
2. Fikira ukiziganda, uamuzi ukatoa,  
Japo ni kama maganda, kwa fani kufanidia,  
Ni jambo mno maonda, nani atakuchezea,  
Na iwe kufanya inda, utenzi kamalizia.
3. Utendapo umetenda, nyuma hutarudishia,  
Jambo lako litawanda, kitabuni kuingia,  
Japo watu kulipenda, wengine kupuuzia,  
Huyo mtenzi katenda, utenzi kamalizia.
4. Huwaje kama maonda, jinsi utachekelea,  
Ukipita unaranda, na kutwa kusimulia,  
Oye kazi mwana ndanda, nani hapo kafikia ?  
Ole na yakija vunda, utenzi kamalizia.
5. Si maridhawa kutenda, kila mtu dahiria,  
Siku mambo yanapinda, anzali kadhihiria,  
Utapata yaloganda, bila ya kutegemea,  
Hata hivyo amepanda, utenzi kamalizia.
6. Na duku duku hutanda, moyo likauzuia,  
Kupandua na kupanda, inda ulo kusudia,  
Hata isiwe kimanda, iwe sumu mno mbaya,  
Japo ni katika tunda, utenzi kamalizia.

*Hamidu R. Tambwe (1970)*